**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**
## BODI YA KOROSHO TANZANIA

### TANGAZO KWA WADAU WOTE WA TASNIA YA KOROSHO NCHINI

Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) inapenda kuwataarifu wadau wote wa Tasnia ya Korosho nchini kwamba usafirishaji wa Korosho ghafi kutoka ghala kuu kwenda Bandari ya Mtwara au katika ghala za wanunuzi za kuhifadhia Korosho utafanyika kwa muda wa saa 24. Ruhusa hii imetolewa maalum kwa ajili ya:-

i. Kupunguza mlundikano wa korosho ghafi katika ghala kuu ili kuruhusu korosho kutoka vyama vya msingi kuingia ghalani kwa wakati.
ii. Kuongeza mzunguko wa malori yaliyopo katika kusafirisha korosho ili kupunguza changamoto ya uhaba wa magari.
iii. Kuwawezesha wanunuzi kuwahi Meli katika Bandari ya Mtwara.
iv. Kukabiliana na changamoto za hali ya hewa, hususan mvua zinazoendelea katika maeneo mbalimbali.

Aidha, ruhusa hii imetolewa kwa Korosho zinazosafirishwa kutoka ghala kuu zilizopo mikoa ya Mtwara,Lindi na Ruvuma Kwenda Bandari ya Mtwara au katika ghala za kuhifadhia Korosho zilizopo Mtwara. Hata hivyo ili kuongeza udhibiti wa ubora wa korosho usafirishaji wa korosho ghafi kutoka kwenye vyama ya msingi (AMCOS) Kwenda Ghala kuu utaendelea kufanyika kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni. Aidha usafirishaji wa korosho kutoka mkoa wa Pwani na mikoa mingine kwenda bandari ya Dar es salaam utafanyika kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa 12 jioni kama ilivyo katika **Mwongozo Na.1 wa Usimamizi wa Masoko na Mauzo ya Korosho Ghafi kupitia Stakabadhi Ghalani Msimu wa 2025/2026.**

Imetolewa na:
**MKURUGENZI MKUU**
**BODI YA KOROSHO TANZANIA**
**08 November 2025**

Korosho Marathon
Eat Cashew,Be healthy